


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

09 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 09 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na

Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

196. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Manyoni Magharibi kwa kushirikiana na Serikali kupitia miradi mbalimbali ikiwemo TASAF wamejenga Zahanati katika Vijiji vya Gurungu, Sanjaranda, Kitopeni, Ipande, Doroto, Itagata, Kalangali, Makule, Mmamagembe na Kintanula lakini mpaka sasa Zahanati hizi hazina Waganga:-

Je, ni lini Serikali itazipatia Zahanati hizo Waganga ili Wananchi wapate huduma kufuatana na Sera yake.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

197. MHESHIMIWA JOSEPH MUSUKUMA (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Meli ya MV Chato

inafanya safari zake kati ya Chato, Senga, Mshalamba, Izumacheli na Nkome. Inapofika Izumacheli huegesha kwenye jiwe kutokana na kukosekana kwa Gati:-

Je, ni lini Serikali itajenga Gati katika Kijiji cha Izumacheli.

198. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ujenzi wa reli kutoka Mtwara – Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma utaanza.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

199. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACPHR) inatumia jengo la TANAPA lililopo Arusha kwa Mkataba wa upangaji baina ya TANAPA na Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano wa Afrika Mashariki ulioanza tarehe 1 Desemba, 2008 kwa kodi ya Dola za Marekani 38,998.89 kwa mwezi:-

Je, kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni nani mwenye jukumu la Haki za Binadamu na nani mwenye jukumu la kulipa kodi ya jengo hilo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA
09 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**